Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Kwanza – Tarehe 13 Juni, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel John Sitta) Alisoma Dua*

## TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, napenda kuwakaribisha rasmi kwenye Mkutano wetu huu wa Nne wa Bunge ambao ni Mkutano wa Bajeti na unaoanza leo Jumanne, tarehe 13 Juni, 2006. Kikao cha Kwanza kikiwa ndiyo hiki.

Ninayo furaha kutambulisha mgeni mashuhuri aliyepo kwenye *Speakers Gallery,* ni Spika Mstaafu Mheshimiwa Pius Msekwa, ambaye amekubali kushiriki nasi. *(Makofi)*

Pili, naomba kutoa taarifa kuwa katika Mkutano wetu wa Bunge wa Tatu, Bunge pamoja na shughuli nyingine ilipitisha Miswada ya Sheria ya Serikali miwili ifuatayo:-

*The Bank of Tanzania Bill 2006* na *The Banking and Financial Institutions Bill, 2006*. Miswada hiyo ilipelekwa kwa utaratibu wa Kikatiba kwa Mheshimiwa Rais ili ipate kibali chake baada ya kupitia katika hatua zake zote za uchapishwaji. Ninayo furaha kukufahamisheni Waheshimiwa Wabunge kwamba Mheshimiwa Rais ametoa kibali chake na sasa Miswada yote miwili ni Sheria za Nchi yaani *The Bank of Tanzania Act, 2006,* unakuwa ni namba 4 ya mwaka 2006 na *The Banking and Financial Institutions Act, 2006* namba 5 ya mwaka 2006. *(Makofi)*

Taarifa ya Tatu, Waheshimiwa Wabunge, ukumbi huu ulikuwa umejengeka katika namna nyingine ya kisasa zaidi ya kulipata jicho la Spika *(catching speakers eye)* ambayo ilikuwa ni kutumbukiza kadi hapa. Napenda kuwathibitishia kwamba kwa mujibu wa Kanuni za Bunge njia zote mbili ile ya kusimama ili Spika akuone na ili akuone kwenye kioo yote ni safi inakubalika. Niseme tu kwamba utaratibu huu wa *electronic* siyo kwamba ni mbadala yote mawili yataendelea.

Mheshimiwa Mbunge ukijisikia jambo limekukera kabisa na huna muda tena wa kutumbukiza tumbukiza kadi wewe simama tu Spika atajua na yote mawili nitayatumia. Kwa hiyo, tuendelee. Katibu Shughuli za leo. *(Makofi)*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 1

### Washauri wa Uchumi wa Rais na Waziri Mkuu

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI** aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu ni maskini sana, je, Mheshimiwa Rais na Waziri Mkuu wanao washauri wa uchumi wa kuelekeza umuhimu wa *Cabinet* ndogo na gharama za *Cabinet* kubwa lenye idadi ya watu 60?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, na mimi niungane na mwuliza swali kwamba namshukuru sana Mwenyezi Mungu kuwa leo kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kuwa wa kwanza kujibu swali katika ukumbi mpya, ukumbi wa kisasa kabisa katika Bara hili la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mbunge wa Chakechake, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania inapiga hatua kubwa katika maendeleo na sio sahihi kudhani ni maskini sana. Kadhalika, ni kweli kwamba idadi ya Mawaziri na Naibu Mawaziri katika Baraza la Serikali ya Awamu ya Nne imefikia 60. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 55 Ibara ndogo ya 1 hadi 3, Rais baada ya kushauriana na Waziri Mkuu amepewa madaraka ya kuteua idadi yeyote ya Wajumbe wa Baraza la Mawaziri na Naibu Mawaziri. Kwa hiyo, ukubwa wa Baraza la Mawaziri utategemea kipaumbele cha Taifa letu kulingana na wakati uliopo na Ilani ya Chama Tawala na kwa sasa ni Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa uteuzi wa Baraza la Mawaziri uliofanyika mwezi Januari, 2006 ulizingatia mahitaji ya kutekeleza *agenda* ya Maendeleo ya Serikali ya Awamu ya Nne. Kwa mfano, Wizara ya Ushirika na Masoko ilivunjwa, Wizara ya Maji na Mifugo ilitenganishwa ili kutoa uzito unaostahili wa sekta nyeti ya Maji na sekta ya Mifugo. Nchi yetu ina mifugo mingi lakini hatujaweza kuitumia fursa hii kikamilifu. Hivyo, kuundwa kwa Wizara ya Mifugo kutasukuma mbele jitihada ya wafugaji ili waweze kufaidika na ufugaji huo. *(Makofi)*

Mheshhimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ziliunganishwa ili kutoa fursa ya Miundombinu kusimamiwa na Wizara moja ya Miundombinu. Aidha, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo iliundwa ili kutoa msukumo katika masuala ya Habari na Michezo kwa Watanzania. Pia Wizara ya Usalama wa Raia na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ziliundwa ili kukidhi mahitaji ya sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba harakati zozote zinazolenga kuleta maendeleo ya haraka kwa wananchi mara nyingi huambatana na gharama kwa umma. La msingi ni tija na maisha bora kwa kila Mtanzania. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba na mimi niungane na wenzangu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sote kuwahi kuingia katika ukumbi mpya wa Bunge hili kama alivyosema Mheshimiwa Rais tunamhakikishia kwamba tutafanya kazi yetu kwa uadilifu na yataonekana matunda ya kuwa katika ukumbi mpya wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, swali moja la nyongeza. Kwa kuwa moja ya tatizo tulilonalo sasa hivi ni uchumi tegemezi yaani Bajeti yetu inategemea *donors* kwa asilimia isiyopungua 48. Hatuoni kuongeza gharama za utumishi kunazidi kutufanya tuzidi kutegemea *donors?*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa gharama wa Serikali hauishii kwa Waziri mmoja au Naibu Waziri mmoja. Haya yote niliyoyasema kwa Wizara zote nilizozitaja hapa kulikuwa na Idara nzima pamoja na Wakurugenzi wake walikuwa wanatenda kazi hizo ambazo hivi sasa zimetengewa Wizara.

Kwa hiyo, kulikuwa na gharama toka zamani kwa mfano, Wizara ya Mifugo kulikuwa na Idara nzima ya Mifugo ambayo ilikuwa inasimamia mifugo nchi nzima, alichofanya Mheshimiwa Rais ni kumteua mtu mmoja ambaye ni Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu ili aweze kusimamia kikamilifu Idara hiyo ya Mifugo. Kwa *agenda* ya sasa kama nilivyosema kwamba tunataka maendeleo kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Sioni kama hiyo ni gharama ambayo hawezi kubebwa na Mtanzania ili kumhakikishia mafanikio makubwa katika nchi yetu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuongeza majibu ya nyongeza kwa yale yaliyojibiwa. Ningependa kwanza kurekebisha kwamba tegemezi ya Serikali kwa *donors* siyo asilimia 48, lakini ni asilimia 41. *(Makofi)*

Na. 2

**Hadhi ya Manispaa ya Morogoro**

**MHE. DR. OMAR M. NIBUKA** aliuliza:-

Kwa kuwa Manispaa ya Morogoro inakua haraka sana kimajengo; na kwa kuwa Manispaa hiyo imezungukwa na Vyuo Vikuu vitatu yaani *Sokoine University, Mzumbe University* na kile cha Kiislam, pamoja na Vyuo vingine ambavyo hutoa Stashahada kama vile Chuo cha Walimu Kigurunyembe na Chuo cha Kilimo Liti na kwa kuwa kwa sasa Manispaa hiyo inahudumia watu wa Mataifa mbalimbali tofauti na Manispaa nyingine nchini:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa sasa wakati umefika wa Manispaa ya Morogoro kupewa hadhi ya Jiji badala ya kubakia Manispaa kama ilivyo sasa?

(b) Je, Serikali haioni kwamba huu ni wakati muafaka kwa Serikali kutoa upendeleo maalum kwa kuboresha miundombinu ya barabara, maji na ukumbi mkubwa wa kisasa ili Manispaa hiyo iweze kuwa na hadhi ya Kimataifa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Omar Mzeru Nibuka, Mbunge wa Morogoro Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro inaweza kupandishwa hadhi kuwa Jiji kwa kufuata sera ya makazi ya mwaka 2000 kwa vigezo vifuatavyo:-

(i) Kuwa na idadi ya watu wasiopungua 500,0000.

(ii) Halmashauri kuwa na uwezo wa kuchangia asilimia 95 ya bajeti yake ya mwaka.

(iii) Kuwe na kumbukumbu za kihistoria.

(iv) Kuwe na vivutio vya kitalii.

(v) Kuwe na shughuli na vikao mbalimbali vya Kimataifa na vya Kitaifa.

(vi) Eneo liwe Makao Makuu ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, Manispaa ya Morogoro ina idadi ya wakazi wapatao 228,863 kulingana na sensa ya mwaka 2002. Manispaa ya Morogoro haina uwezo wa

kipato cha kuchangia asilimia 95 ya Bajeti yake ya mwaka. Kwa mfano, katika mwaka 2004/2005 Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro Bajeti yake ilikuwa jumla ya shilingi bilioni 5.1. Vyanzo vyake vya mapato ilikuwa ni shilingi 663,837,997 ambapo ni sawa na asilimia 7.8. Aidha, katika mwaka wa fedha 2005/2006 Bajeti ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ilikuwa ni shilingi bilioni 7.5 ambapo mchango wa Halmashauri ni shilingi milioni 744,710,028 sawa na asilimia 10.17.

Mheshimiwa Spika, kipato cha wakazi wa Manispaa ya Morogoro kwa wastani ni shilingi 337,032. Aidha, Manispaa ya Morogoro ina eneo la kilometa za mraba 265. Urefu wa barabara za Manispaa hiyo ni jumla ya kilometa 325 zikiwa kilometa 12 tu za lami, kilometa 76 ni za changarawe na kilometa 237 ni za udongo ambazo hazipitiki nyakati zote kwa mwaka. Pia kumbukumbu za kihistoria zilizopo ni chache kwa mfano Makaburi ya Mtawala Kingo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba watalii wote wanaokwenda katika Mbuga ya Mikumi ambayo ipo Wilaya ya Kilosa na Milima ya Udzungwa ambayo iko Wilaya ya Kilombero na Milima ya Uluguru hupitia katika Manispaa ya Morogoro. Lakini kutokana na uwezo mdogo wa Manispaa hiyo bado haijaweza kuwa kitovu cha utalii cha kuvutia mikutano ya Kimataifa na ya Kitaifa. Hivyo, Manispaa hiyo haijaweza kukidhi baadhi ya vigezo vinavyotakiwa ili kupandishwa hadhi kuwa Jiji.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa fedha za kuboresha miundombinu ya barabara na maji kwa Halmashauri zote bila upendeleo ikiwa pamoja na Manispaa ya Morogoro. Napenda kutoa wito kwa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuboresha miundombinu na kudhibiti matumizi yake ya fedha. Aidha, Manispaa inashauriwa kujenga mazingira mazuri ili kuvutia wawekezaji.

**MHE. DR. OMAR M. NIBUKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Naomba nimuulize Naibu Waziri wa TAMISEMI kwamba kama itatokea wananchi wa Morogoro kipato chao kikawa kizuri na idadi ya wakazi ikafikia hiyo 500,000 kama alivyosema. Je, Serikali iko tayari kutubadilishia badala ya kuwa Manispaa ikawa Jiji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi kwamba wakitimiza vigezo vilivyotajwa Serikali itakuwa tayari kubadilisha hadhi ya Manispaa ya Morogoro kuwa Jiji. *(Makofi)*

Na. 3

**Vitalu vya Uwindaji - Liwale**

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa asilimia hamsini na tatu (53%) ya eneo la Wilaya ya Liwale yenye ukubwa wa kilometa za mraba 39,000 linatumika kwa shughuli za uwindaji wa kitalii:-

(a) Je, kuna vitalu vingapi vya uwindaji, vinamilikiwa na Kampuni zipi na kwa muda gani?

(b) Je, Serikali imepata kiasi gani cha fedha kutokana na biashara hiyo kati ya mwaka 2000 na 2005, na Kampuni husika zimetumia kiasi gani na kwa miradi gani ya maendeleo katika Wilaya ya Liwale?

(c) Je, ni sababu zipi zilizoifanya *GTZ* kusitisha shughuli zake katika uhifadhi na ni nani anayeendeleza shughuli hizo sasa?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Katika Wilaya ya Liwale kuna jumla ya vitalu 14 vya uwindaji wa kitalii. Vitalu hivyo vinamilikiwa na kampuni 5 kama ifuatavyo:-

(i) *Gerald Pasanis Safari Corporation Ltd.* vitalu sita (6) tangu mwaka 1978.

(ii) *Barlette Safari Corporation Ltd.* vitalu vitatu (3) tangu mwaka 1984.

(iii) *Tanzania Wildlife Corporation Ltd.* vitalu viwili (2) tangu mwaka 1978.

(iv) *African Bush Co.Ltd.* vitalu viwili (2) tangu mwaka 1995.

(v) *Tanganyika Wildlife Safari Corporation Ltd.,* kitalu kimoja (1) tangu mwaka 1978.

Mheshimiwa Spika, vitalu hivi viligawiwa tena kwa mara ya mwisho mwaka 2005 hadi 2009.

(b) Kati ya mwaka 2000 na 2005 jumla ya *USD 1,515,467.00* zilikusanywa kutokana na uwindaji wa kitalii katika Wilaya ya Liwale.

Katika kipindi hicho, kampuni za uwindaji wa kitalii zinazowinda katika Wilaya ya Liwale zimetumia kiasi cha jumla ya shilingi 76,159,730.00 katika kuchangia miradi mbalimbali ya maendeleo katika Wilaya hiyo, ikiwa ni pamoja na kujenga shule za sekondari katika vijiji vya Barikiwa, Kikulyungu na Chimbuko.

(c) *GTZ* ni Shirika la Maendeleo la Ujerumani ambalo shughuli zake hapa nchini zilijikita katika kusaidia uhifadhi wa wanyamapori kwa kupitia miradi mbalimbali. *GTZ* ilianza shughuli zake hapa nchini mwaka 1988 na ilimaliza muda wake mwaka 2005. Baada ya muda wake kumalizika Shirika hilo lilisitisha mchango wake katika uhifadhi. Kwa sasa Wizara kupitia Idara ya Wanyamapori ndiyo inayosimamia miradi yote iliyokuwa ikisimamiwa na *GTZ.*

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Nashukuru kwa majibu mazuri aliyotoa Naibu Waziri. La kwanza, lakini nataka kumhakikishia kwamba *GTZ* wakati kabla hawajasitisha mipango yao ya maendeleo ya Wilaya ya Liwale walikuwa wameahidi kusaidia ukarabati wa Boma ya Liwale kwa kutoa milioni 8 ili waanze kukarabati na kwamba Serikali ya Ujerumani ingesaidia kutoa fedha hizo. Je, sasa hivi hali hiyo ikoje, nani anashughulikia kukarabati jengo hilo la Boma la Liwale ili liweze kutumika kwa ajili ya ofisi?

La pili, kuna barabara kati ya Ilonga katika Wilaya ya Ulanga iendayo Ndapata katika Wilaya ya Liwale barabara hii imefungwa kwa muda mrefu sana eti kwa sababu tu kuna Hifadhi za wanyamapori. Je, mbona zipo barabara kama ile inayopita Serengeti na ile inayopita Mikumi huko hakuna wanyamapori? Tunaomba barabara hiyo ifunguliwe haraka iwezekanavyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, swali la nyongeza lile la pili, naona linastahili kuulizwa kipekee kwa sababu linaleta suala jipya kabisa linahusu ruksa ya barabara. Lakini majibu ya swali la kwanza la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi shughuli za uhifadhi zilizokuwa zikifanywa na Shirika la *GTZ* sasa zitafanywa na Idara ya Wanyamapori. Kwa hiyo, hata hiyo barabara anayoizungumzia tutaangalia pia uwezekano wa kutengenezwa na Idara ya Wanayampori.

Na. 4

**Madini ya Dhahabu Mwime, Kata ya Mwendakulima**

**MHE. JAMES D. LEMBELI** aliuliza:

Kwa kuwa utafiti wa madini ya dhahabu katika eneo la Mwime Kata ya Mwendakulima, Wilayani Kahama, umekaribia kukamilika na kwamba mipaka ya

migodi imebainishwa na maeneo ya makazi na mashamba ya wananchi wa eneo hilo yamo ndani ya mipaka ya migodi. *(Makofi)*

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani za tahadhari kuhakikisha kwamba wananchi ambao maeneo yao yameonekana kuwa ndani ya eneo la mgodi yakiwemo makaburi wanalipwa fidia inayostahili kuepuka migogoro inayoweza kujitokeza?

(b) Je, Serikali imeweka taratibu gani za kuhakikisha yale yote yaliyomo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM kuhusu stahili za wananchi wanaoishi na kupakana na migodi yanatekelezwa ikiwa ni pamoja na suala la ajira?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mbunge wa Kahama, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo ya jumla kuhusiana na suala hili kama ifuatavyo:-

Kampuni ya *Pangea Minerals Limited* imekuwa ikifanya utafutaji wa dhahabu katika eneo la Buzwagi lililoko Wilayani Kahama mara baada ya leseni ya utafutaji mkubwa wa madini kutolewa kwa Kampuni ya Kitanzania ya *Madaba Minerals Limited* tarehe 29 Juni, 1992. Kampuni ya *Pangea Minerals* sasa hivi inaendelea na utafutaji wa madini hayo katika eneo hilo ili kugundua mashapo zaidi ya madini kabla ya kuanza shughuli za uchimbaji. Kampuni hiyo ilianza upembuzi yakinifu (*feasibility study*) wa mradi huo mwezi Desemba , 2005 na kuukamilisha mwezi Mei, 2006. Kwa sasa kampuni hiyo inaendelea na kuchambua athari za uchimbaji madini kwa mazingira pamoja na kuandaa mpango wa uthibiti wa mazingira *(EMP),* kazi ambazo zitakamilika mwezi Juni, 2006. Kazi hizi zinajumuisha uainishaji wa maeneo yenye mashamba, makaburi, mazao na mali nyingine zinazomilikiwa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya ufafanuzi huo, napenda sasa kujibu swali la msingi la Mheshimiwa James Daudi Lembeli, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Sheria ya Madini ya mwaka 1998 inaruhusu leseni za kutafuta na kuchimba madini kutolewa katika eneo lolote ambalo halina leseni nyingine ya madini. Aidha, kifungu Na. 95 cha sheria hiyo kinamtaka mmiliki wa leseni ya utafutaji na uchimbaji wa madini kupata kibali cha maandishi kutoka kwa mtu au mamlaka inayotumia ardhi hiyo (*surface right*) kabla ya kuanza shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini katika eneo hilo. Kifungu hiki cha sheria kinatoa fursa nzuri ya kuepusha kuwepo kwa migogoro ya matumizi ya ardhi baina ya wananchi na wamiliki wa leseni za madini.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi wamiliki wa leseni za madini hufanya makubaliano na wenye maeneo husika kwa mujibu wa kifungu Na. 96(3) cha Sheria ya Madini ya mwaka 1998. Endapo wahusika watashindwa kufikia muafaka kuhusu kiwango cha fidia, wanaweza kufungua shauri kwa Kamishna wa Madini au katika Mahakama kwa mujibu wa kifungu Na.101(1) cha Sheria ya Madini ili kupata ufafanuzi

wa kisheria na kwa hatua zaidi za fidia. Aidha, kwa mujibu wa sheria za fidia, Wizara ya Ardhi ndiyo yenye dhamana ya kutoa utaratibu na viwango stahili vya fidia.

Katika kuhakikisha stahili za wananchi wanaoishi jirani na migodi, wamiliki wa mgodi kwa kusaidiwa na Serikali waliunda Kamati Shirikishi (*Resettlement Working Group*) ambayo inajumuisha wajumbe kutoka Wilayani, Vijijini na Kampuni ya *Pangea Minerals Limited.* Wajumbe wa Wilaya ni Mkurugenzi Mtendaji, Mthamini wa Wilaya pamoja na Maafisa wa Wilaya wa Kilimo, Maendeleo ya Jamii, Elimu, Misitu, Ardhi, Afya, Mipango, Mipango Miji na Biashara.

Mheshimiwa Spika, wajumbe wengine ni Maafisa Watendaji wa Kata na Vijiji pamoja na wawakilishi wawili kutoka kila kijiji, mmoja akiwa mwanamke na mwingine mwanaume. Vijiji vinavyohusika ni Chapulwa, Mwendakulima na Mwime. Kamati hii imesaidia sana katika kuwatambua wananchi ambao wanastahili fidia na kiasi cha fidia wanachostahili. Jumla ya wananchi 3,500 watafidiwa katika maeneo yao. Kati ya hao 1,500 watahamishwa kutoka kwenye makazi yao ya sasa.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Ilani ya uchaguzi ya CCM, Wizara yangu inaendelea kuhamasisha wamiliki wa migodi mikubwa ya uchimbaji madini nchini kutoa kipaumbale katika utoaji wa ajira kwa wananchi wenye sifa zinazostahili ambao wanaishi katika maeneo yanayopakana na migodi hiyo hususan kazi mbalimbali ambazo hazihitaji utaalam maalum. Hii itasaidia kuinua kipato cha wananchi wengi wanaoishi katika maeneo hayo.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali la nyongeza.

Kwa kuwa tayari kampuni hii ya *Pangea* imeanza kutoa ajira hata kabla haijapewa leseni ya uchimbaji, Serikali itachukua hatua gani kuhakikisha kwamba ajira hizo ambazo nyingi ni za nje ya eneo hili zinasimamishwa hadi hapo kampuni hii itakapokuwa imepewa leseni?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa James Lembeli, kama ifutavyo:-

Kwanza napenda kumhakikishi Mheshimiwa Lembeli kwamba katika kipindi hiki leseni ya uchimbaji katika eneo la Buzwagi haitatolewa mpaka kamati ambayo inapitia mikataba ya madini itakapomaliza kazi yake na katika kuhakikisha na kuhamasisha kwamba makampuni ya madini yanatoa ajira kwa wananchi ambao wanaishi katika maeneo ya migodi.

Mheshimiwa Spika, tarehe 1 na 2 Julai, 2006 Wizara yangu inakutana na makampuni yote makubwa ya madini katika kuwaeleza kwanza sera ambayo iko ndani ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi, itawaeleza misimamo ya Serikali ya awamu ya nne na kuhakikisha kwamba migodi yote ambayo inafanya kazi ndani ya nchi yetu inafanya kazi kwa manufaa ya Watanzania ambao ni wananchi halisi wa hapa, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi nashukuru Mungu kwamba tuna ukumbi mpya. Swali langu la nyongeza.

Kwa kuwa sheria inakubali kwamba wale wakazi wa pale wanaweza kufanya makubaliano juu ya fidia ambayo pia fidia ni pamoja na fidia kwa Halmashauri kwa kupoteza nguvukazi ya watu 1,500 ambao hawatatumia hiyo ardhi labda kwa kulima pamba na mambo mengine. Je, kwa nini Serikali isihamasishe au Serikali isiwashauri Halmashauri wakakakubaliana kuwa wanapewa angalau asilimia mbili au tatu ya mapato yote yatakayopatikana zaidi kwa migodi mipya?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Cheyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali analoliuliza linahitaji mtazamo mpana zaidi juu ya faida ya nchi inayopata kutoka kwenye sekta ya madini na kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu vizuri sana, ndiyo kazi ambayo tunaifanya hivi sasa na tunatarajia kuihitimisha mwanzoni mwa mwezi Julai, 2006. Lakini pia kabla ya wakati huo ipo faida Halmashauri ilipaswa kuipata ambapo hapo nyuma walikuwa hawaipati lakini sasa hivi Serikali kupitia vikao ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu amevifanya pamoja na wamiliki wa migodi hii

Kwa sasa hivi Serikali imeweza kuwahimiza wenye migodi hii walipe si chini ya dola 200,000 kwa kila Halmashauri kwa mwaka fedha ambazo walipaswa wazilipe, hapo zamani walikuwa hawazilipi.

Mheshimiwa Spika, lakini kiujumla swali alilolisema kama nilivyosema awali ni swali linalohitaji mtazamo mpana zaidi na ndiyo tunalishughulikia kuhakikisha kwamba nchi hii inafaidika vizuri zaidi kwa madini ikiwa ni pamoja na mambo ambayo yanapaswa kwenda kwenye Halmashauri zetu hapa nchini.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa kuzingatia muda inabidi tuendelee swali linalofuata, Mheshimiwa Ahmed Ally Salum.

Na. 5

**Mradi wa Maji Kutoka Ziwa Victoria**

**MHE. AHMED ALLY SALUM** aliuliza:-

Kwa kuwa mradi wa kuvuta maji toka Ziwa Victoria unaendelea vizuri na unapita kwenye vijiji vingi vya Tarafa ya Nindo katika Jimbo la Solwa:-

(a) Je, Serikali imekusudia kupeleka maji kwenye kila kaya na vijiji ambako bomba la maji hayo linapita?

(b) Je, mabwawa yanayojengwa kutokana na mradi huo kwa ajili ya mifugo, yatajengwa kwenye kila Kata au Vijiji vingapi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Jimbo la Solwa, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mradi wa bomba kuu la maji kutoka Ziwa Victoria hadi miji ya Kahama na Shinyanga ambao unatekelezwa na Wizara yangu, unapitia kwenye jumla ya vijiji 54 vikiwemo vya Solwa, Mahingula, Mwiseme na Mwasekage vyenye wakazi wapatao 12,300 katika jimbo la Solwa. Maeneo mengine yanayopitiwa na bomba hilo ni kata za Mwamashimba, Ilujamate, Lubili na Mwawile katika Wilaya za Kwimba na Misungwi Mkoa wa Mwanza na Salawe, Iselamagazi, Mwantini, Pandagichiza, Lyabukande, Bulige, Kinaga na Nangaya katika Wilaya za Shinyanga Vijijini na Kahama Mkoa wa Shinyanga. Vijiji hivyo vina jumla ya wakazi 167,500 kwa hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekusudia kupeleka maji katika kila kijiji ambako bomba kuu litapita. Katika awamu ya kwanza ambayo inatekelezwa hivi sasa, kila kijiji kitawekewa tawi la bomba na kituo cha kuchotea maji *(kiosk).*

Aidha, matanki 38 yenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya lita milioni 2 yatajengwa katika baadhi ya vijiji hivyo ili kuhakikisha kuwa maji yanapatikana wakati wote. Katika awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi huo ambayo itaanza 2007/2008, Wizara yangu kwa kushirikiana na vijiji na Halmashauri za Wilaya husika, inakusudia kulaza mabomba ya kusambaza maji ili kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi. Ulazaji huo wa mabomba utazingatia kigezo kilichowekwa kwenye Sera ya Maji ya kupeleka huduma ya maji kwa umbali usiozidi mita 400 kutoka kila kaya kwenye maeneo ya vijijini.

(b) Mheshimiwa Spika, mradi huu haujengi mabwawa bali utajenga mahori ambao tunasema ni *cattle troughs* kwa ajili ya mifugo takriban 1,620,000 iliyopo kwenye vijiji ambavyo bomba kuu linapita. Mahori hayo yatajengwa katika kila kata au kijiji kwa kuzingatia idadi ya mifugo pamoja na uwezo wa malisho ya kila kijiji ili kuepusha athari za mazingira. Hivyo, idadi kamili na maeneo yatakapojengwa mahori hayo itaainishwa kabla ya kuanza ujenzi wa awamu ya pili, mwaka 2007/2008.

**MHE. AHMED ALLY SALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri yenye matumaini lakini katika majibu yake sikusikia Kata ya Mwakitorio. Kata ya Mwakitorio bomba limepita umbali wa kilomita tatu au nne na inaponyesha mvua huwa Kata hiyo huwa imetengwa inakuwa kama kisiwa muda wa miezi sita. Sasa je, Serikali haioni umuhimu wa kupeleka huduma ya maji katika Kata ya Mwakitorio?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa majibu ya swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Solwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunapoanza kutekeleza mradi wowote ule tunaanza kwanza kufanya upembuzi yakinifu ili uweze kufikisha huduma mahali ambapo umekusudia na kwa gharama zinazokusudiwa. Kwa hiyo, hivi ndivyo ilivyofanyika kwa mradi huu mkubwa sana wa kutoa maji ziwa Victoria kwenda katika maeneo ambayo yametajwa. Sasa kwa eneo hilo analolizungumzia Mheshimiwa Mbunge tutawasiliana naye ili tujue kama inaweza kuhudumiwa katika awamu ya pili baada ya kufanya upembuzi yakinifu sababu nia ni kufikisha maji kwa watu wengi zaidi na ikiwezekana wote.

Kwa hiyo, pale inapowezekana tutafanya, lakini kama ipo nje ya mpango wenyewe itabidi tufanye mpango mwingine ili wananchi hao waweze kuhudumiwa.

Na. 6

**Shirika la Uwekezaji la Taifa *(NICO)***

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa ni muda sasa tangu Shirika la Uwekezaji la Taifa *(NICO)* lianzishwe:-

(a) Je, ununuaji wa hisa umeliingizia shirika hilo fedha kiasi gani hadi sasa?

(b) Je, mgawanyo wa faida kwa wana hisa utaanza lini na unafuata utaratibu gani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *NICO* ilikusanya jumla ya shilingi 12,947,290 kwa uuzaji wa hisa kwa kutumia mtindo wa kuuza hisa moja kwa moja kwa wananchi *(Initial Public Officer- IPO)* kwa hatua mbili kama ifuatavyo:-

(i) Katika *IPO* ya kwanza iliyoanza tarehe 13/11/2004 na kufungwa tarehe 31/012005, zilikusanywa shilingi 4,496,320,000.

(ii) Shilingi 8,450,970,000 zilikusanywa katika *IPO* ya pili iliyofanyika tarehe 5/9/2005 mpaka 23/9/2005 ambayo ililenga kununulia hisa za ziada na *NMB* ambazo zilishindikana kununuliwa na *Exim Bank* na *TCCIA*.

(b)Kwa mujibu wa Sheria Na. 212 ya usajili wa makampuni, mgao wa faida unafanywa kulingana na maamuzi ya wanahisa katika mkutano mkuu wa mwaka *(AGM)* kwa kufuata matakwa ya Katiba ya kampuni. Kwa msingi huo, katika Mkutano Mkuu wa mwaka 2005 uliofanyika tarehe 28/01/2006, ambao faida kabla ya kodi kwa mwaka huo ilikuwa shilingi 144,312,595 iliamuliwa kwamba kwa kuwa kampuni inahitaji kupanua mtaji wake gawio la faida kwa wanahisa litafanyika mwishoni mwa mwaka unaofuata

baada ya kutathimini ni kiasia gani cha kubakiza kama mtaji na kipi cha kugawa kwa wanahisa.

Na. 7

**Kuondolewa kwa Kodi ya Mafuta ya *JET A - 1***

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika Bajeti ya mwaka 2005/2006 iliondoa kodi ya mafuta ya *JET A-1* yanayotumiwa kwenye ndege:-

(a) Je, kuanzia tarehe 1 Julai, 2003 hadi tarehe 31 Machi, 2004 ni kiasi gani cha mafuta ya *JET A-1* na mafuta ya taa kiliingizwa nchini?

(b) Je, mahitaji ja *JET A-1* ni lita ngapi kwa mwezi?

(c) Je, ni kiasi gani cha ya *JET A-1* kiliingizwa nchini katika mwaka wa fedha wa 2004/2005?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAFA H. MKULO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mbunge wa Kwamtupura, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2005/2006. Serikali iliondoa kodi ya mafuta aina ya *JET A-1* yanayotumiwa kwenye ndege ili kuleta usawa katika ushindani kwa faida ya Kampuni za ndege za hapa nchini. Katika kipindi cha kuanzia tarehe 1 Julai,2005 hadi tarehe 31 Machi, 2006 mafuta yaliyoingizwa nchini ni kama ifuatavyo:-

(i) Mafuta ya ndege *JET A-1* lita 102,291,505 na mafuta ya taa lita ni 58,783,484.

(b) Mheshimiwa Spika, mahitaji ya mafuta aina ya *JET A-1* kwa mwezi yanatofautiana kutegemea idadi ya ndege katika mwezi husika. Kwa mfano wakati wa msimu wa utalii ndege huwa nyingi kuliko msimu ambao si wa utalii na hivyo matumizi huongeazeka. Hata hivyo wastani wa matumizi ya *JET A-1* kwa mwezi ni takribani lita 11,365,723.

(c) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, kiasi cha mafuta kilichoingizwa hapa nchini ni kama ifuatavyo:-

(i) Mafuta ya ndege *JET A-1* lita 125,961,666 na mafuta ya taa lita ni 105, 996,163.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kwa mujibu wa takwimu zilizotoka imeonekana kumekuwa na ongezeko la mafuta ya *JET A-1* baada ya kuondoa ushuru na kwa kuwa mafuta hayo yanaweza kutumika kama mbadala kama mafuta ya taa. Je, Serikali haina mashaka yoyote kuhusu ongezeko hilo?

Pili, Serikali baada ya kujitoa katika biashara hii ya mafuta je, ni taasisi gani inayojua hasa kiasi cha mafuta kinachoingizwa nchini na yanayotumika pamoja na yale yanayopita kama *transit?*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swalia la Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, makampuni ya mafuta nchini yanawajibika kutoa taarifa za uingizaji wa mafuta nchini kwa Shirika la Taifa la Mafuta nchini *(TPDC)* na shirika hili kuleta taarifa Wizarani. Lakini pia *TRA* nayo ndiyo inayofuatilia kwa karibu zaidi siku hadi siku mafuta yanayoingizwa nchini kwa maana ya ulipaji kodi.

Kuhusu wasiwasi ambao unaweza ukawepo kwamba mafuta haya *JET A-1* yanaweza yakatumika kwa sababu nyingine baki ya kutumika kwa ndege, wasiwasi huo unaeleweka, unafahamika Serikalini na unafatiliwa kwa karibu. Kwa sababu kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema ni kweli kwamba mafuta haya badala ya kuyatumia kwenye ndege pia unaweza ukayatumia kama mafuta ya taa na kwa sababu hiyo Serikali imekuwa ikifuatilia kuhakikisha kwamba watu wafanye biashara ya mafuta hawatumii mwanya huo kuagiza mafuta wakisingizia kwamba ni ya ndege lakini huyauza madukani kama mafuta ya taa na hivyo kukwepa ushuru. Kwa hiyo, ni suala ambalo linafahamika na linafuatiliwa kwa karibu.

Na. 8

**Utendaji wa Shirika la *NSSF***

**MHE. AHMED M. SHABIBY** aliuliza:-

Kwa kuwa Shirika la *NSSF* ni shirika la wafanyakazi ambalo lina uwekezaji mkubwa kuliko shirika lingine nchini na kwa kuwa kila mfanyakazi na kibarua hukatwa mshahara wake kwa lazima:-

(a) Je, wafanyakazi ambao ni wadau wa Shirika hilo wanashirikishwaje katika maamuzi ya uwekezaji?

(b) Je, kwa nini mapato ya Shirika hilo hayako wazi kwa wanachama na wadau wake?

(c) Je, wanachama na wadau wa Shirika hilo wanafaidika vipi na uwekezaji wa Shirika hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Shabiby, Mbunge wa Gairo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Wafanyakazi ambao ni wadau wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii wanashirikishwa katika maamuzi ya uwekezaji kupitia uwakilishi wao katika Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa *NSSF*. Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa *NSSF* ni ya utatu, ambapo Serikali, waajiri na wafanyakazi ambao ni wanachama wa Mfuko huo wana uwakilishi sawa. Wawakilishi wa wafanyakazi katika Bodi ya Wadhamini hupatikana kupitia Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi *(TUCTA)*ambapo majina matatu hupendekezwa kwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ambaye ndiye mwenye mamlaka ya uteuzi. Vyama vya Waajiri pia huchagua wawakilishi wao watatu ambao huunganishwa na wajumbe watatu kutoka Serikalini na kukamilisha idadi hiyo ya utatu.

Mheshimiwa Spika, maamuzi yote kuhusu uwekezaji huwasikilishwa kwenye Bodi ya Wadhamini kwa uchambuzi na maamuzi. Ushiriki wa Wafanyakazi katika maamuzi ya uwekezaji ni kwa kupitia uwakilishi kwenye Bodi ya Wadhamini.

(b) Mheshimiwa Spika, Mapato ya Shirika la Hifadhi ya Jamii huwekwa wazi kwa wanachama wake kupitia hesabu za Shirika *(Audited Accounts)* zinazotolewa kila mwaka. Hesabu za Shirika ambazo pamoja na mambo mengine huonyesha mchanganuo wa vyanzo mbalimbali vya mapato na kiasi kilichopatikana kila mwaka hukaguliwa na wakaguzi wa nje *(External Auditors)* kama ilivyoainishwa kwenye Sheria ya *NSSF* Na. 28 ya mwaka 1997 kifungu 69 kifungu kidogo 2. Mahesabu hayo huwasilishwa kwenye Kamati ya Bunge la Kudumu ya Maendeleo ya Jamii kila mwaka ambapo huchambuliwa na kutolewa maelekezo.

Aidha, Taarifa za Hesabu za Shirika *(Annual Report)* huchapishwa na nakala kupelekwa Bungeni kwa ajili ya Wabunge wote. Aidha, nakala hizo hupelekwa kwa vyama huru vya wafanyakazi waajiri wanaochangia mfuko wa *NSSF* taasisi mbalimbali na maktaba za taifa. Hali kadhalika Taarifa za Hesabu za mwaka za Shirika la *NSSF* *(Published Accounts)* zinapatikana kwa matumizi ya umma pia. Katika taarifa hizi mchanganuo wa mapato ya Shirika huonyeshwa kikamilifu.

(c) Mheshimiwa Spika, Shirika huwekeza katika nyanja mbalimbali (*Investment Portfolio)* ili kulipatia Shirika faida. Faida inayopatikana hutumika kuboresha mafao kwa wanachama wake. Mafao yatolewayo na Shirika ambayo ni ya muda mrefu na muda mfupi huongezeka mwaka hadi mwaka. Pia mafao hayo huboreshwa ili kuendana na mwenendo na hali ya uchumi. Mafao ya muda mrefu ni pamoja na pensheni baada ya kustaafu *(Retirement Pension),* Penseni ya Ulemavu *(Invalidity Pension)* na Penseni kwa

wategemezi *(Survivors Pension).* Mafao ya muda mfupi ni yale uzazi, kuumia kazini, matibabu na msaada wa mazishi.

Mafao ya muda mrefu hufanyiwa marekebisho mara kwa mara kutokana na mfumuko wa bei na kupanda kwa kima cha chini cha mshahara.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) katika Mkataba Na. 102 kwa mwaka 1952 *(ILO Convention No. 102 of 1952)* imeainisha mafao tisa yanayotakiwa kutolewa na taasisi yoyote ya Hifadhi ya Jamii duniani. Mpaka sasa *NSSF* inatoa mafao saba na kuifanya kuwa taasisi pekee katika nchi zilizo kusini mwa jangwa la Sahara kutoa mafao mengi kuliko taasisi nyingine yoyote katika bara la Afrika. (*Makofi*).

**MHE. DR. JAMES M. WANYACHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kuwa makato ya *NSSF* huchukua muda mrefu mpaka mtu apate pensheni na kwa kuwa thamani ya fedha yetu imekuwa ikiporomoka kwa kasi kubwa. Je, Shirika hilo linachukua tahadhari gani kuhakikisha kwamba mtu anapopata pensheni haadhiriki kwa sababu ya kuporomoka kwa thamani ya fedha yetu?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mbunge wa Serengeti, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba Shirika la *NSSF,* linafanya mapitio ya kila mwaka kuhakikisha kwamba kushuka kwa thamani ya fedha kunatiliwa maanani wakati wa kuangalia mafao ya wafanyakazi na nimeeleza kwamba mafao haya yanabadilika mwaka hadi mwaka kulingana na uwezo wetu wa shilingi *against other currencies*. Kwa hiyo, ni jambo ambalo linatazamwa kwa kina.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi aidha, namshukuru Naibu Waziri, kwa majibu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wafanyakazi hawa wanakatwa fedha na kwa kuwa mfuko huu tayari umeonyesha kukopesha watu mbalimbali. Je, ni kwa nini mifuko hii haiandai utaratibu wa kuwakopesha wafanyakazi wenyewe ili waweze kupata mtaji wa kuendesha maisha yao?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, kama ifuatavyo:-

Kimsingi mifuko hii siyo mifuko ya uwekezaji ni *Pension Funds,* inafanya kuwekeza ili ipate faida iweze kuwalipa vizuri zaidi wanachama wake mafao yao. Lakini hata hivyo niseme tu kwamba sasa sheria tunaitizama upya kwa mujibu wa sera yenyewe ya hifadhi ya jamii ili kuhakikisha kwamba wanachama wananufaika na fedha zao wanazochangia katika *NSSF*. (*Makofi*)

Na. 9

**Matumizi Yasiyofaa ya Mifuko ya Mashirika ya Pensheni Nchini**

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni pamejitokeza matumizi yasiyoridhisha kwa mifuko ya mashariki ya pensheni hapa nchini na hivyo kupelekea kuwepo kwa mvutano wa taarifa mbalimbali kwa vyombo vya habari juu ya matumizi hayo mabaya ya fedha za wanachama na kwamba mashirika hayo yamejiingiza sana katika kuwekeza katika miradi mbalimbali ya majengo pasipo kuwepo na utaratibu mahsusi wa uwekezaji kwa fedha hizo za wanachama ambao mafao yao kila siku hayaboreshwi ipasavyo na hivyo kupelekea maisha duni baada ya kustaafu:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuanzisha mamlaka ya kudhibiti mashirika ya Mifuko ya Pensheni (*Regulatory Authority)* katika uendeshaji wake na pia kuwepo na ukomo wa Bodi za Wadhamini katika kupitisha maamuzi makubwa ya uwekezaji wa fedha na wanachama ambao umesababisha kuwepo kwa mtikisiko wa dhamana yaliyonayo dhidi ya mali za wanachama wa mifuko hiyo?

(b) Je, kwa nini Benki Kuu isiruhusiwe kuwa na sheria ya kuyadhibiti mashirika hayo kama moja ya Taasisi za Fedha hapa nchini kwa vile sasa malengo makubwa yamekuwa ni uwekezaji wa fedha za mifuko hii?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DANIEL NICODEM NSANZUGWAKO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mbunge wa Busega, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 2003 Serikali ilipitisha Sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii. Lengo la Sera hii ni pamoja na kuweka mazingira mazuri ya maendeleo katika Sekta ya Hifadhi ya Jamii pamoja na mambo mengine, Sera inaelekeza mambo yafuatayo:-

(a) Kutungwa kwa sheria ya kusimamia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nchini.

(b) Kuanzishwa kwa chombo cha kusimamia Sekta ya Hifadhi ya Jamii nchini.

(c) Kuwepo kwa mwongozo wa matumizi ya fedha zitokanazo na michango ya wanachama katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza sera hii, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii, imekamilisha Sheria ya Kusimamia Sekta ya Hifadhi ya Jamii ambayo pamoja na mambo mengine itaainisha chombo cha kusimamia Sekta ya Hifadhi ya Jamii nchini ikiwa ni pamoja na Mifuko ya Pensheni. Mara baada ya

maandalizi ya sheria hii kukamilika Serikali itaandaa Muswada wa Sheria na kuuwasilisha katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Mashirika ya Pensheni ni aina moja ya mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo lengo lake kuu ni kutoa kinga dhidi ya majanga yanayosababishwa na mtu kupoteza uwezo wake wa kufanya kazi na hivyo kushindwa kujipatia kipato, kwa mfano uzee, ulemavu na kadhalika. Kinga hii hutolewa kwa kutoa mafao mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mwanzo kwenye swali Na. 8, uwekezaji si kazi ya msingi ya mifuko ya Hifadhi ya Jamii, bali kuwekeza katika katika vitega uchumi kumeruhusiwa kisheria kwa lengo la kuipa mifuko hiyo uwezo wa kutekeleza majukumu yake ya kimsingi ya kutoa mafao ya muda mfupi na pia mafao ya muda mrefu kwa wanachama wake. Kwa misingi hii, mifuko ya Hifadhi ya Jamii itaendelea kuwekeza kwa kuzingatia mwongozo wa uwekezaji wa fedha za mifuko ya Hifadhi ya Jamii nchini, unaoandaliwa sambamba na sheria ya kusimamia Sekta ya Hifadhi ya Jamii kama ilivyoelekezwa katika sera ya Taifa ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo Mifuko ya Hifadhi ya Jamii itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kutoa mafao bora yanayotosheleza na kukidhi mahitaji ya wanachama wake.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishaeleza hapo awali, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inakamilisha maandalizi ya sheria na suala la mgawanyiko wa majukumu miongoni mwa wadau katika kusimamia utekelezaji wa sheria hii litazingatiwa kikamilifu. Ni matarajio ya Wizara yangu kuwa sheria hii itakapokamilika, Benki Kuu kama mmoja wa wadau wakuu na wadau muhimu katika sekta hii itakuwa na jukumu kubwa na la msingi katika kusimamia sheria hii.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ingawa muda unaonekana kama umefika ni saa nne, lakini kwa kuwa tulianza na matangazo, nimekadiria kwamba niongeze dakika tano ili tuweze kumaliza vizuri kipindi hiki cha maswali. Swali la nyongeza Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni.

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda tu kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa vile Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba, uwekezaji katika Mifuko hii si suala la msingi na hivi karibuni kumetokea changamoto juu ya suala la uwekezaji kupitia mifuko hii. Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya suala zima hili ambalo halina tija kwa wanachama wa Mfuko wenyewe na kwa watanzania wote?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO):** Mheshimia Spika, hayo maneno ambayo yamesemwa kuhusu hasa Mfuko huu wa *NSSF*, mengi kwa asilimia kubwa hayana ukweli kwa sababu Mfuko wa *NSSF* una uwezo wa aslimia 73 sasa kuweza kumudu majukumu yake kwa sasa. Matatizo mengine madogo madogo ni ya kibiashara na hayo

malumbano ambayo mmeyasikia mengine yako mahakamani. Kwa hiyo tusubiri mahakama zitakapokuwa zimetoa uamuzi wake.

**SPIKA:** Mheshimiwa, Zitto Kabwe, swali la nyongeza.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la uwekezaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii hasa *NSSF* na *PSPF,* limesababisha ugomvi mkubwa miongoni mwa wafanyabishara wakubwa wawili nchini, Yusuf Manji na Reginald Mengi, na kwa kuwa tayari mahakama imetoa uamuzi…

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu...

**SPIKA:** Ndiyo, utaratibu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Spika, swali analouliza bado liko mahakamani, kwa hiyo naomba asiruhusiwe kuuliza.

**MBUNGE FULANI:** Safi sana!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, taarifa, mwezi uliopita…

**MBUNGE FULANI:** Limeisha!

**SPIKA:** Tangu nilipoyasoma maswali haya huwa najiandaa vizuri tu. Nilipata ushauri wa kisheria kwamba kesi ya msingi bado iko mahakamani. Iliyoondolewa ni shauri lililohusu utaratibu ili kufikia ile kesi ya msingi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, bado hili liko mahakamani.

Na. 10

**Hati za Umiliki wa Ardhi kama Dhamana ya Mikopo**

**MHE. ZAYNAB M. VULU** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nichukue nafasi hii katika Ukumbi Mpya kuwa mtu wa mwisho kuuliza swali, lakini mwisho wa swali ndio mwanzo wa swali. Je, kuna mkakati gani wa kutoa hati za umiliki wa leseni kama zilivyotolewa Mkoa wa Dar es Salaam kwenye baadhi ya Wilaya katika maeneo yasiyo rasmi kwa wakazi wa vijiji ili nao waweze kuitumia kama dhamana katika kuchukua mikopo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikwisha kuanza kutekeleza Sheria ya Ardhi Na. 4 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 za mwaka 1999 tangu mwaka 2001.

Vile vile iliandaa na kuanza kutekeleza mkakati wa kutekeleza Sera na Sheria za Ardhi nchini *(Strategic Plan for the Implementation of the Land Laws)*. Wadau wa kutekeleza mkakati huu ni pamoja na Serikali Kuu, Halmashauri za Miji na Wilaya, vyombo vya habari na Mashirika yasiyoyakiserikali. Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 kifungu Na. 23 Halmashauri nchini zinayo mamlaka ya kutambua wananchi waliojenga nyumba kwenye maeneo yasiyo hatari na kutoa leseni za makazi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Halmashauri za miji na Wilaya zimeanza kutekeleza kazi hiyo zikiwemo Jiji la Dar es Salaam, Mwanza na Manispaa ya Dodoma. Kwa maeneo ya vijijini, Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999 imeweka utaratibu wa kupima mipaka ya vijiji, kutoa cheti cha ardhi ya kijiji pia kupima mashamba ya wanavijiji na kutoa Hati na Haki miliki za kimila.

Mheshimiwa Spika, kutokana na utekelezaji, imeonyesha kuwa kasi ya upimaji wa viwanja nchini imeongezeka na baadhi ya Wilaya zimeteuliwa kuwa za mfano katika kutekeleza Sheria ya Ardhi ya Vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 vijiji 6,000 vimepimwa na Serikali itaendelea kupima vijiji vilivyobaki nchi nzima. Serikali imepima vijiji vya mfano Wilaya ya Mbozi na Iringa Vijijini na vile vile imepima mashamba ya wanavijiji na kutoa Hati za Hakimiliki za Kimila. Halmashauri za Miji na Wilaya zingine zinatakiwa kuiga mfano huu. Baadhi ya Halmashauri za Miji na Wilaya zimeiga mfano huu na zimeanza kutoa hati za Hati za haki miliki za Kimila. Wilaya hizo ni pamoja na Handeni, Kilindi na Babati.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia Hati za Hakimiliki za Kimila, wanavijiji wanaweza kujipatia mikopo kutoka Mabenki na taasisi mbalimbali za fedha.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha na maswali yamekwisha. Ninalo tangazo. Kuna taarifa hapa ya kikao, Katibu wa *Tanzania Women Parliamentary Group*, Mheshimiwa Eliatta Namdumpe Switi, anawatangazia wanachama wote yaani Wabunge Wanawake wote kuwa leo tarehe 13 Juni, 2006, kutakuwa na kikao kitakachofanyika hapa Bungeni katika Ukumbi wetu wa zamani wa Bunge saa 11.00 jioni. Mnaombwa tafadhali nyote muweze kufika kwa sababu kuna wageni wanaokutana nanyi kuzungumza masuala muhimu yanayowahusu ninyi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa orodha ya shughuli za leo, hapa ndio tumefikia mwisho kwa shughuli za leo. Kwa hiyo, naliahirisha Bunge hadi kesho asubuhi saa 3.00.

*(Saa 4.09.45, Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatano, Tarehe 14 Juni, 2006 saa 3.00 asubuhi)*